MAMLAKA YA HALI YA HEWA
TANZANIA
JARIDA LA HALI YA HEWA


**Na: 32. Msimu wa Kilimo 2018/19 Tathmini ya Kipindi cha Agosti 1-10, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Agosti 11-20, 2019**

**Muhtasari**

- Mvua za nje ya msimu zinazotarajiwa zitaathiri ukaushaji na utunzaji wa mazao.
- Hali ya ukavu ikiambatana na upepo mkali katika maeneo ya ukanda wa pwani itapelekea kupungua kwa maji.
- Wafugaji wanashauriwa kuwa na matumizi endelevu ya vyanzo vya maji na kufuata ushauri unaotolewa na maafisa ugani.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 1-10, 2019

Katika kipindi hiki cha dikadi migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo eneo mwa kusini mwa Dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika kidogo hivyo kuimarisha mkondo wa mgandamizo mkubwa wa hewa wa Afrika mashariki. Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo eneo la kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kudhoofika kidogo na hivyo kusababisha ukanda wa mvua kuendelea kubaki kaskazini zaidi mwa nchi. Uwepo wa joto la bahari la juu ya wastani katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi kulisababisha kuongezeka kwa joto husussan nyakati za usiku katika eneo la mashariki mwa nchi. Katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (pwani ya Angola) joto la bahari la juu kidogo ya wastani lilionekana,wakati katika eneo la pwani ya Somalia kulikuwa na joto la bahari la chini kidogo ya wastani. Mwelekeo wa mkondo wa mgandamizo mkubwa wa hewa wa Afrika mashariki kuja nchi kavu ulisababisha upepo kuvuma kutoka kusini mashariki na kuchangia kuongezeka kwa joto hususan nyakati za usiku katika maeneo mengi ya nchi.




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Agosti 1- 10, 2019

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 1-10, 2019

Kwa kipindi hicho maeneo mengi ya nchi yalikua makavu isipokua kwa baadhi ya maeneo machache ya ukanda wa ziwa Viktoria hususan mkoa wa Mara na maeneo ya pwani ya kaskazini hususan mkoa wa Tanga ambayo yamepata mvua za nje ya msimu. Kiasi cha mvua kilichopimwa kwa mkoa wa Mara ni kati ya 26 mm na 50 mm na mkoa wa Tanga ni kati ya 201mm hadi 249 mm kama inavyojionesha kenye kielelezo.

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 1-10, 2019

Katika maeneo mengi ya nchi wakulima wamemaliza shughuli za uvunaji wa mahindi kwa msimu wa mvua wa Machi hadi Mei 2019. Wakulima wanaendelea zaidi na shughuli za ukaushaji , uhifadhi wa mazao na kuandaa mashamba kwa msimu ujao wa mvua za vuli. Upatikanaji wa maji na malisho ya mifugo uliendelea kupungua kiasi kutokana na hali ya ukavu na upepo eneo la ukanda wa pwani.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 1-10, 2019

Kina cha maji kwenye mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vililiendelea kupungua kidogo kwa maeneo mengi ya nchi kutokana na hali ya ukavu na upepo.

.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 11-20, 2019

Katika kipindi hiki cha dikadi migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo eneo la kusini mwa Dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo eneo la kaskazini la dunia inatarajiwa kudhoofika, hivyo kusababisha vipindi vya upepo mkali katika ukanda wote wa pwani. Ukanda wa mvua unatarajiwa kuendelea kubaki kaskazini zaidi mwa nchi. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kusababisha mvua nyepesi katika maeneo ya ukanda wa pwani. Aidha, joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika maeneo ya pwani ya Angola na Somali. Hata hivyo, uwepo wa mkondo wa mgandamizo mkubwa wa hewa wa Afrika mashariki unatarajiwa kuendelea kusababisha vipindi vya upepo mkali utakaovuma kutoka kusini hadi kusini mashariki katika ukanda wa pwani yote.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 11-20, 2019

Maeneo ya kanda ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kuwa na vipindi vifupi vya mvua na ngurumo katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) na Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) kunatarajiwa kuwa na vipindi vifupi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kuwa na mawingu kiasi.

## MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 11-20,2019

Mvua za nje ya msimu zinazotarajiwa zinaweza kuathiri ukaushaji na utunzaji wa mazao. Hali ya ukavu inayotarajiwa ikiambatana na upepo mkali itapelekea kupungua kwa kiasi kidogo cha maji. .Wafugaji wanashauriwa kuwa na matumizi endelevu ya vyanzo vya maji na malisho huku wakifuata ushauri unaotolewa na maafisa ugani.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 11-20, 2019.

.

Kina cha maji kwenye mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kupungua kiasi katika maeneo ya ukanda wa pwani kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa ikiambatana na upepo mkali. Watumiaji wa maji wanashauriwa kuwa na matumizi endelevu ya vyanzo vya maji vilivyopo.

*Jarida limetayarishwa na:*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

***S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz***